OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

..............................

**HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE**

Simu: 028-2227148
Fax: 028-2227140

E-mail: ded.karagwe@kagera.go.tz
ded@karagwedc.go.tz

S.L.P 20,

**KARAGWE.**

**15/04/2019**

**YAH: TANGAZOKWA WANANCHI WOTE**

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA MWAKA HUU 2019 KUTAKUWA NA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA.

WANANCHI WOTE MNATANGAZIWA KUJIANDAA NA UCHAGUZI KWA MAANA YA KUSHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA KUPIGA KURA NA KUJITOKEZA KUGOMBEA NAFASI MBALIMBALI.

**NAFASI ZITAKAZO GOMBEWA NI PAMOJA NA**

i. MWENYEKITI WA KIJIJI
ii. MWENYEKITI WA KITONGOJI
iii. WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI
iv. WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI VITI MAALUM

Kati ya wajumbe watakao chaguliwa, Idadi ya wanawake itakua nusu au zaidi ya wajumbe wote ambapo wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji hawatapungua 15 na hawatazidi 25.

**SIFA ZA WAGOMBEA NI KAMA ZIFUATAZO;-**

- AWE RAIA WA TANZANIA
- AWE MKAZI WA KAWAIDA WA ENEO HUSIKA
- AWE MTU YEYOTE MWENYE UMRI KUANZIA MIAKA 21 NA KUENDELEA
- AWE ANAJUA KUSOMA NA KUANDIKA KISWAHILI AU KIINGEREZA
- AWE MWENYE KIPATOHALALI
- AWE MWANANCHAMA NA ADHAMINIWE NA CHAMA CHA SIASA KILICHOSAJILIWA
- ASIWE NA UGONJWA WA AKILI NA

- AWE HAJAPATIKANA NA HATIA NA KUPATA ADHABU YA KIFUNGO CHA MIEZI SITA AU ZAIDI.

**SIFA ZA MPIGA KURA NI KAMA IFUTAVYO ;-**

- AWE RAIA WA TANZANIA MWENYE UMRI WA MIAKA 18 NA KUENDELEA
- AWE AMEANDIKISHWA NA MWENYE KITAMBULISHO CHA KUPIGA KURA
- AWE MKAZI ANAYEISHI KWENYE ENEO LA KIJIJI AU KITONGOJI HUSIKA.

AIDHA, WANANCHI WOTE MNAKUMBUSHWA KUJIANDAA NA UCHAGUZI HUO NA IKUMBUKWE KWAMBA KUPIGA KURA NI HAKI YA KILA MWANANCHI MWENYE SIFA HIVYO MNAOMBWA KUJITOKEZA NA KUSHIRIKI KIKAMILIFU.

**Imetolewa na :-**

Godwin M.Kitonka
**MKURUGENZI MTENDAJI ( W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA,**
**<u>KARAGWE.</u>**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KARAGWE